

**MRADI WA KINGA DHIDI YA MAAMBUKIZI YA VVU NA ATHARI ZA UKIMWI
KWA WASICHANA BALEHE NA WANAWAKE VIJANA**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Maendeleo ya Jamii)

UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania imepata usaidizi wa Fedha kutoka Mfuko wa Dunia (*Global Fund-GF*) kwa ajili ya kuendeleza miradi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) na athari za UKIMWI nchini kwa kipindi cha Januari 2018-Desemba 2020.

Mradi wa GF kwa Tanzania Bara umelenga vipaumbele (thematic areas) 11 kuhusu kinga dhidi ya VVU na athari za UKIMWI.

Mradi wa GF utatekelezwa na Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchi nzima kwa kipindi cha miaka mitatu (Januari 2018-Desemba 2020).

Mradi wa Kinga dhidi ya VVU na athari za UKIMWI kwa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana ndani na nje ya shule (Adolescent Girls and Young Women-AGYW in schools and out of schools)

MRADI WA VVU na UKIMWI

- Mradi huu utatekelezwa katika mikoa 3 ya majaribio kwa kipindi cha Januari 2018-Desemba 2020 kwa Tanzania Bara; katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma na Singida.
- Walengwa wakuu wa Mradi huu ni Wasichana Balehe na Wanawake Vijana wenye umri kati ya miaka 10-24 walio ndani na nje ya shule.
- Watekelezaji wa Mradi wa AGYW ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), NACP, AMREF, TASAF, TAYOA na WAMJW.

TACAIDS itaratibu utekelezaji wa mradi wa AGYW.

LENGO LA MRADI

Lengo Kuu la Mradi ni kuwasaidia wasichana walioko shuleni kuendelea kupata elimu na walio nje ya mfumo wa elimu kupata mbinu mbadala za kujikimu kimaisha wakiwa salama dhidi VVU na UKIMWI.

MALENGO MAHSUSI

1. Kutekeleza programu za VVU/UKIMWI katika mabadiliko ya tabia (Behavioral Change).
2. Kutekeleza Programu za VVU/UKIMWI za Kitabibu (Bio-Medical).HTC

3. Kutekeleza Programu za VVU/UKIMWI kwa masuala Mtambuka (Structural).
4. Kutekeleza Programu za VVU/UKIMWI kwa misingi ya Jinsia na Haki za Binadamu (Human rights and Gender) GBV

WADAU WAKUU WA MRADI GF

| | | |
|----|---|--|
| 1. | Wizara ya Fedha na Mipango | <ul style="list-style-type: none"> • Kuingia Mkataba na Mfuko wa Dunia (GF) na Waratibu wakuu wa GF. Fedha yote inapitia hapo. |
| 2. | Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) | <ul style="list-style-type: none"> • Kuitisha na kuratibu mikutano yote ya wadau wa AGYW |
| 3. | Mpango wa Taifa wa Kuzuia UKIMWI (NACP) | <ul style="list-style-type: none"> • Waratibu wa Programu za UKIMWI za kitabibu za Serikali na taasisi zisizo za Kiserikali zikiwemo Mipango Mikakati, Ufuatiliaji na • Tathmini (M&E), Uratibu wa sekta ya afya katika VVU, Kifua Kikuu kwa Makundi Maaalumu. Manunuzi ya vifaa tiba vya UKIMWI. • Kufanya tafiti za awali (Baseline surveys), • Kutengeneza na kutoa miongozo ya mafunzo, Kusimamia ubora wa mafunzo yatakayotolewa na wadau |
| 4. | Wizara-Idara ya Maendeleo ya Jamii | <ul style="list-style-type: none"> • Kutambulisha Mradi kwa Wadau, Mapitio ya nusu mwaka ya utekelezaji wa mradi na tathmini ya mwisho ya mradi AGYW |

| | | |
|----|--|---|
| 5. | Wizara-Idara ya Afya; Afya ya Uzazi na Huduma za Watoto (Reproductive & Child Health Services) | <ul style="list-style-type: none"> Elimu ya Uzazi Salama, Kansa ya njia ya Kizazi, utambuzi na matibabu kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia |
| 6. | OR-TAMISEMI | <ul style="list-style-type: none"> Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi katika Halmashauri na uratibu wa vikao vya mapitio ya mipango ya UKIMWI ya Halmashauri. Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya UKIMWI kila mwisho wa mwaka. |

WADAU WAKUU WA MRADI GF

| Na. | TAASISI | MAJUKUMU KATIKA GF |
|------------|---------------------------------------|---|
| 7. | Vyuo Vikuu/ Taasisi za utafiti | Tafiti na kuratibu utekelezaji wa Tafiti |
| 8. | Kamati za Afya za Mikoa (RHMT) | Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya UKIMWI katika Halmashauri na uratibu wa vikao vya mapitio ya mipango ya UKIMWI ya Halmashauri. Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya UKIMWI kila mwisho wa mwaka. |
| 9. | Halmashauri (LGAs) | Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya UKIMWI katika vituo vya kutolea huduma, Kuratibu Mikutano ya UKIMWI na Kifua Kikuu, Mafunzo kwa watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma na gazi ya Jamii na kuratibu vikao vya kisheria vya kamati za UKIMWI na Kifua Kikuu katika Halmashauri. |

| | | |
|-----|---|--|
| 10. | Wadau Wengine wa UKIMWI na Kifua Kikuu | Kutoa usaidizi wa Kitaalamu kwa Kamati ya Afya ya Mkoa (RHMT), Kamati ya Afya ya Wilaya (DHMT) na Kituo cha Ushauri na Upimaji (CTC) katika Halmashauri zilizoainishwa ili kufikia (90-90-90); ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mradi na kujenga uwezo wa watekelezaji wa mradi. |
| 11. | Bohari Kuu ya Madawa (MSD) | Kununua, kuhifadhi na Kusambaza vitendanishi na vifaa tiba |
| 12. | Damu Salama (NBTS) | Kuhakikisha upatikanaji wa damu salama |

WADAU WENGINE WA MRADI GF AGYW

| Na. | TAASISI | MAJUKUMU KATIKA GF |
|-----|---------|---|
| 13 | TASAF | <ul style="list-style-type: none"> ▪ Kutoa Mafunzo kwa wawezeshaji ngazi ya Halmashauri juu ya ukusanyaji takwimu za washiriki wa mradi wa AGYW ▪ Kusimamia zoezi la ukusanyaji takwimu za washiriki wa Mradi wa AGYW ▪ Kutoa mafunzo ya uingizaji takwimu kwenye mfumo wa kompyuta kwa waingiza takwimu (data entry clerks) ▪ Kutoa mafunzo ya uhakiki wa takwimu za washiriki. ▪ Kuchakata takwimu za washiriki ili kutengeneza malipo ngazi ya TASAF Makao Makuu ▪ Kutuma ruzuku kwa washiriki wa mradi wa AGYW ▪ Kurekebisha taarifa za washiriki wa mradi wa AGYW itakapobidi |

WADAU WENGINE WA MRADI GF AGYW

| | TAASISI | MAJUKUMU KATIKA GF |
|----|---------|--|
| 14 | AMREF | <ul style="list-style-type: none"> • Kupokea fedha kutoka GF na kuzipatia Taaasisi zisizo za kiserikali ikiwepo TAYOA • Amref itatekeleza mradi wa huduma rafiki kwa wasichana balehe na wanawake vijana mkoa wa Singida (Singida MC, Singida DC& Iramba DC) • Kutoa mafunzo ya malezi na makuzi kwa wazazi wa wasichana balehe na wanawake vijana (Parenting Training) • Kuwapatia pedi (sanitary pads) wasichana walioko shule na nje ya mfumo wa elimu • Kutoa elimu ya ujasiliamali na stadi za maisha kwa walio nje ya mfumo wa elimu • Kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU |
| | TAYOA | <ul style="list-style-type: none"> • TAYOA itatekeleza mradi wa huduma rafiki kwa wasichana balehe na wanawake vijana mkoa wa Dodoma (Bahi DC, Kondoa DC, Kongwa DC & Mpwapwa DC) na Morogoro (Ulanga DC, Malinyi DC & Ifakara DC) • Kutoa mafunzo kwa waelimishaji rika (Peer Educators Training) • Kutoa mafunzo ya malezi na makuzi kwa wazazi wa wasichana balehe na wanawake vijana (Parenting Training) • Kuwapatia pedi (sanitary pads) wasichana walioko shule na nje ya mfumo wa elimu |

MAENEO YA UTEKELEZAJI

1. DODOMA

Mradi utatekelezwa katika kata na vijiji vyote ambavyo vimefikiwa na programu ya TASAF ya kunusuru kaya maskini katika H/W za Bahi, Kongwa, Mpwapwa na H/Mji Kondoa.

2. MOROGORO

Mradi utatekelezwa katika kata na vijiji vyote ambavyo vimefikiwa na programu ya TASAF ya kunusuru kaya maskini katika H/W za Malinyi, Ulanga na Ifakara.

3. SINGIDA

Mradi utatekelezwa katika kata na vijiji vyote ambavyo vimefikiwa na programu ya TASAF ya kunusuru kaya maskini katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, H/W za Singida na Iramba.

UHITAJI WA MRADI (KWANINI WASICHANA BALEHE 10-25)

Sensa ya Watu na Makazi (2012) kwa Tanzania inaonesha kundi la vijana chini ya miaka 24 ni takribani asilimia 63 ya idadi ya Watanzania wote.

Maambukizi mapya ya VVU kwa jamii yote yameendelea kushuka ikijumuishwa na kundi la vijana wenye umri kati ya miaka 15-24 kwa asilimia 18 kwa kipindi cha miaka 3 iliyopita.

Hata hivyo, uwiano wa maambukizi mapya ya VVU kwa vijana wenye umri kati 15-24 yameendelea kuwa juu kwa asilimia 31 ukilinganisha na maambukizi yote (2015 Spectrum estimates).

Kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kwa vijana balehe na vijana (10–24) ni 40%. Kati ya hayo maambukizi, 80% yanatoka kwa kundi la Wasichana Balehe na Wanawake Vijana (THIS, 2016/17).

Hatari ya Maambukizi ya VVU kwa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana yanachangiwa na sababu kuu 3 ambazo ni; sababu za kitabia (behavioral), za kibaiolojia (biological) na mtambuka (structural).

Umaskini wa kipato katika kaya unawaweka Wasichana Balehe na Wanawake Vijana katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU kwa kushiriki ngono zisizo salama ili kupata kipato.

Kundi hili linajumuisha wasichana kutoka katika kaya maskini ambao wamekatisha masomo kutokana na umaskini.

Wasichana waliokatisha masomo hawapati mbinu mbadala za kujikimu kimaisha zikiwemo stadi za maisha na ujasiriamali; hivyo kuwa kwenye hatari ya kushiriki biashara ya ngono ambayo ni kichocheo kikubwa cha maambukizi ya VVU.

Kutokana na kufanya ngono zisizo salama, kundi hili lipo kwenye hatari ya kupata mimba za utotoni, kuolewa katika umri mdogo na kufanyiwa vitendo vingine vya ukatili vinavyochangia uwezekano wa kupata maambukizi ya VVU.

Kutokana na changamoto hizo, Serikali kupitia usaidizi wa GF, imeamua kuanzisha na kuendeleza programu za VVU na UKIMWI kwa kundi la Wasichana Balehe na Wanawake Vijana kupitia afua zifuatazo:-

- a. Kubadili tabia,
- b. Programu za upimaji wa VVU na matibabu ya UKIMWI,
- c. Programu za Afya ya Uzazi,
- d. Programu za kuondoa umaskini wa kipato na
- e. Programu nyingine mtambuka.

Katika kupunguza umaskini wa kipato, mradi huu utalenga kaya maskini zaidi kama zilivyoanishwa na zitakavyokuwa zikiainishwa na programu ya kunusuru kaya maskini inayoratibiwa na TASAF, kwa kutumia mfumo wa utoaji wa ruzuku kwa kaya maskini zaidi (cash tranfer).

Programu ya kunusuru kaya maskini inalenga watoto waliopo shuleni na wale walio nje ya mfumo wa shule ili kutoa huduma zinazoendana na mahitaji kwa kuzingatia umri wao kupitia kaya maskini.

Kwa ujumla, wasichana Rika na wasichana Balehe (*Adolescent Girls and Young Women*) wapo kwenye hatari kubwa kuendelea kupata maambukizi ya VVU, lakini upatikanaji wa huduma za VVU na UKIMWI umeendelea kuwa duni. Pia, Elimu ya Afya ya Uzazi kwa kundi hili haijapewa kipaumbele ikilinganishwa na watu wazima (TDHS 2015-16).

PROGRAMU ZITAKAZOTEKELEZWA NA MRADI

Programu za mabadiliko ya tabia zitajumuisha:-

- i. Programu za Afya ya uzazi,
- ii. Kuondoa Ubaguzi na Unyanyapaa kwa wanaoishi na VVU,
- iii. Programu ya malezi na makuzi,
- iv. Programu ya utaalumu na usaidizi katika kuendeleza taaluma na vipaji kwa walengwa waliopo shuleni na nje ya mfumo wa shule,
- v. Mbinu za uhamasishaji jamii na kuondokana na mila zenye madhara na masuala ya unyanyasaji wa kijinsia.

Programu za kitabibu zitajumuisha:-

- i. Programu za kondomu kwa ujumla wake
- ii. Huduma za upimaji wa VVU na matibabu ya UKIMWI,
- iii. Huduma kwa wenza wanaoishi na VVU,
- iv. Huduma za afya ya uzazi,

Huduma kwa wahanga wa unyanyasaji wa kingono zikiwemo huduma za kisaikolojia

- Programu zinazohusu masuala mtambuka:-
 - i. Kupanua wigo wa utoaji wa huduma rafiki za VVU na UKIMWI na huduma za Afya ya uzazi kwa kundi hili.
 - ii. Kuwajengea uwezo watoa huduma za afya ili kuendelea kutoa huduma rafiki kwa kundi hili.
 - iii. Kuimarisha uwezo wa kiuchumi, ikiwemo kuwapatia fedha za ruzuku wasichana rika na wasichana balehe wanaotoka katika kaya maskini zaidi.
 - iv. Kuwapatia pedi (*sanitary pads*) Wasichana Balehe na Wanawake Vijana walioko shule na nje ya mfumo wa elimu.
 - v. Kwa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana (walioko nje ya mfumo wa elimu) watapatiwa elimu ya ujasiriamali na stadi za maisha pamoja na mtaji (*seed money*) kwa ajili ya kuanzisha shughuli za uzalishaji mali.

PROGRAMU YA HAKI ZA BINADAMU NA JINSIA

- Changamoto za VVU na UKIMWI kuhusu masuala ya haki za binadamu na Jinsia, zitaainishwa na kuandaliwa afua katika maeneo yafuatayo; eneo la kisera, programu ya haki za binadamu na jinsia kwa kuhusisha jamii na eneo la kuimarisha utoaji wa huduma:-
 - i. *Eneo la kisera:* Programu italenga katika kufanya ushawishi ili kubadili sheria ya kuzuia na kukabiliana na UKIMWI, sheria Na. 28 ya 2008, ikiwa pamoja na kupunguza umri wa kupima VVU kwa hiari hadi kufikia miaka 15 kutoka 18 ya sasa.
 - ii. *Utekelezaji wa programu kwa kuhusisha jamii;* Programu italenga kuamsha ari katika jamii, viongozi wa dini na viongozi wa kimila ili kujadili changamoto za haki za binadamu na jinsia ikiwemo mila zenye madhara zinazoliweka kundi la AGYW katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU.

iii. *Utekelezaji wa programu katika kuimarisha eneo la utoaji huduma:-*

- Mafunzo kwa watoa huduma za afya na waelimisha rika yatatolewa ili kuweza kutoa huduma bora kwa wahanga wa ukatili wa kingono zikiwemo utambuzi wa mapema wa ukatili huo na mfumo wa upatikanaji wa huduma kwa waathirika katika jamii husika.
- Kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya ili kuwezesha utoaji wa huduma rafiki kwa Wasichana rika na wasichana balehe katika masuala ya VVU na elimu ya afya ya uzazi.
- Kufanya mapitio ya miongozo iliyopo ya zana za kufundishia (*IEC materials*) ili kuandaa mwongozo jumuishi kwa ajili ya kundi la Wasichana Balehe na Wanawake Vijana
- Kufanya utambuzi wa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana waliopatiwa mafunzo wenye weledi na uwezo ili kutoa huduma kwa wenzao katika vituo rafiki vitakavyoainishwa

JUKUMU LA WIZARA KATIKA KUANDAA JAMII KWA UTEKELEZAJI WA MRADI

- Jukumu la WAMJW (Maendeleo ya Jamii) ni kuutambulisha mradi wa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana na kuandaa mazingira rafiki na wezeshi ya utekelezaji wake.
- Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa watashiriki katika utekelezaji wa Mradi huu baada ya kupata uelewa.
- Maafisa Maendeleo ya Jamii watatumia taaluma na ujuzi walionao ili kuiandaa jamii kwa kuzingatia majukumu ya msingi ya Maafisa hao kama ifuatavyo:-

MAJUKUMU MENGINE YA MAAFISA MAENDELEO YA JAMII

- Kuratibu na kuandaa mazingira rafiki na wezeshi ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya jamii katika ngazi zote.
- Kuwezesha jamii kushiriki katika kubuni, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini mipango na miradi yao ya maendeleo.
- Kuelimisha na kuhamasisha wananchi ili kushiriki katika utekelezaji wa kazi za maendeleo mfano; programu za kiuchumi, usafi wa mazingira, ujenzi wa shule na zahanati.

- Kuhamasisha na kuwawezesha wananchi kutambua fursa zilizopo na kuzitumia ili kupanga mbinu za kujiletea maendeleo.

MAJUKUMU YA MAAFISA MAENDELEO YA JAMII

- Kuwezesha upatikanaji na kutoa wa mafunzo kwa Viongozi wa ngazi mbalimbali na vikundi vya maendeleo yakijumuisha; uongozi na mbinu shirikishi za jamii.
- Kuwa kiungo kati ya Wadau wa Maendeleo na Jamii katika kusaidia utekelezaji wa shughuli za maendeleo.
- Kuhamasisha uundwaji wa vikundi vya kijamii na vya kiuchumi.
- Kuratibu na kusimamia shughuli za Mashirika na Asasi zisizo za Kiserikali kwa Kijamii.

Kuratibu shughuli za kupambana na VVU na UKIMWI

- Sambamba na utekelezaji wa Majukumu hayo; Wizara na Wadau wa Maendeleo ya Jamii katika Mkutano Mkuu wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii wa Novemba, 2017 Mjini Dodoma walibainisha maazimio makuu 4 kwa kada ya Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo:-
 - a. Kuunganisha mifumo ya uhamasishaji jamii ili iweze kuamsha Ari ya ushiriki katika uzalishaji kwenye Sekta mbalimbali ili kuongeza mnyororo wa thamani ya bidhaa zinazozalishwa.
 - b. Kuamsha Ari ya jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo zitakazochochea uboreshaji wa huduma za jamii zikiwemo ujenzi wa miundo mbinu ya barabara, maji, afya na elimu ili kufikia uchumi wa viwanda.
 - c. Kuratibu na kuunganisha juhudi za wananchi /vikundi vya kiuchumi na taasisi wezeshi kama vile VETA, SIDO, FDCs, TBS, TFDA, CDTIs, Taasisi za fedha na Mifuko ya uwezesaji kiuchumi
 - d. Kuamsha Ari ya jamii kupiga vita mila zenye madhara na kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Katika utekelezaji wa Programu hii, ni jukumu la Maafisa Maendeleo ya Jamii kuhakikisha kwamba miradi ya aina hii inaoanishwa na majukumu ya msingi ya kada ya Maendeleo ya Jamii ya kuelimisha, kuhamasisha na kuikinga jamii dhidi ya athari zinazotokana na harakati za kujitafutia maendeleo.

WAJIBU WA MIKOA NA HALMASHAURI KATIKA KUTEKELEZA MRADI

Je, Mkoa na Halmashauri ina wajibu gani katika kuandaa mazingira rafiki na wezeshi ya kutekeleza Mradi huu?

MAENEO YA KUFANYIA KAZI BAADA YA WARSHA - ACTION POINTS

Baada ya kupata ufahamu kuhusu mradi huu. Je, ni maeneo gani ya kufanyia kazi ili kuandaa mazingira rafiki na wezeshi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii?

ASANTENI